بسم الله الرّحمن الرحيم

18/Safar/1427H=18/March/2006Ad,Madinatul Rassuuli llahi -swalla alayhi wasallam- Saudi Arabia.Makala Namba 1.

# HII NDIYO DAAWA YETU

## JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIHI

## ATHARI MBAYA YA UZUSHI KATIKA UISLAMU.

Amesema Swahaba Mtukufu Abdullahi Ibn Umar Ibn al-Khattabi:

كل بدعة ضلالة وان رآها الناس حسنا

“Bidaa zote ni upotevu hata kama watu wataziona kuwa ni nzuri”.

Ameitaja athari hii Imamu al-Bayhaqy katika kitabu chake al-Mad'khali ukurasa 191, na Imamu al-Laalakai katika kitabu chake Shar'hu usuulil- I'tiqaadi ukurasa 126.

MUANDISHI;

AL AKH QASSIM MAFUTA QASSIM.

## UTANGULIZI

Sifa zote njema, ni stahiki ya Allah Bwana wa viumbe wote, na swala na salamu zimfikie Mtume wetu Muhammad swalla llaahu alayhi wasallam Mbora waviumbe wote, na pia ziwafikie jamaa zake, na Maswahaba zake wote, na walio waandamia hao kwa wema, mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya utangulizi.

Ndugu yangu muislamu,napenda kuitumia fursa hii adhimu kukumbusha jambo moja muhimu sana, ambalo Allah -Jalla Jalaaluh- na Mtume wake -swalla llaahu alayhi wasallam- wamelipa uzito na kulisisitiza mara nyingi kwa waislamu wote, jambo ambalo ndiyo sababu ya izza na ushindi kwa waislamu, jambo lenyewe ni mshikamano katika dini juu ya kamba moja ya Allah, na kuachana na mambo yote yanayoleta farka.

Bila shaka Muislamu yoyote atakubaliana na mimi kwamba katika mambo ambayo yanaupa unyonge umma huu wa kiislamu, na kuonekana kuwa ni dhalili katika macho ya maadui wa uislamu, na mpaka uislamu kufikia kuwa unachezewa, ni kukosekana mshikamano wa kweli juu ya kamba ambayo tumeamrishwa na Allah -Jalla Jalaaluh- tushikamane nayo.

Na bila shaka, kamba yenyewe ni dini ya Allah -Sub'haanahu wata'alaa- ambayo ina ncha mbili kuu ambazo ni;

Kitabu cha Allah -Ta'alaa- na Sunnah za Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-

Na bila shaka, ndugu yangu muislamu utakubaliana na mimi kwamba ziko sababu za kimsingi zilizo pelekea kwenye mtafaruku huu wa Waislamu, na si kwamba hivi ndivyo walivyo umbwa waislamu.

Kama hivyo ndivyo basi, ili mambo yetu yatengenee, na izza na heshima irudi katika umma huu, ni sharti tuyajue mambo hayo yanayo tufarikisha,
na pia tukubali kwamba mambo hayo ndiyo maradhi yenyewe ya asili, na huu mtafaruku ni alama tu ya kwamba sisi tuna magonjwa mazito ima ya siri au yadhahiri.

Pia tukubaliane kwamba, kupiga kelele tu, na kusema;

WAISLAMU TUSHIKAMANE, NA TUACHE FARKA ZETU !! Na hapo hapo tukayafumbia macho maradhi hayo ambayo ndiyo kiini cha mtafaruku huu, kelele hizo hazito saidia kitu.

Ni kama vile mgonjwa wa kifua kikuu anayewakera watu kwa kikohozi chake, badala ya kumpeleka Hospital, ili kumpatia tiba muafaka, unampa tangawizi ili kukata kikohozi, tatizo hapo si kikohozi, bali tatizo ni hilo gonjwa lenyewe ambalo ndilo kiini cha kikohozi hicho.

Kwa hivyo basi ndugu yangu Muislamu, ni wajibu wangu mimi na wewe kujua tuna maradhi gani ambayo yanatusumbua?

je ni Saratani? au ni Utapiamlo?

Tafadhali isome makala hii kwa umakini, pamoja na kuyatafakari yaliyomo na wala usiwe na jazba wala papara ya kuwa hukumu watu hapo ndipo utakapo yagundua maradhi yanayo tudhoofisha na utaigundua kinga yake na tiba yake.

Na kutokana na uzito wa maradhi hayo, afadhali ingelikuwa miili yetu ndiyo iliyopatwa na maradhi hayo, labda huwenda jamaa, ndugu na watoaji wa misaada ya kibinaadamu wakitaifa, na wakimataifa wangetusaidia kwa kuzingatia ubinaadamu wetu.

Lakini kwa bahati mbaya kinacho umwa ni kiwiliwili cha uislamu,uislamu ambao maadui wake hawalali,wanakwenda mbio kila uchao kuhakikisha uislamu unakufa duniani ! kwa kutumia mbinu tofauti, kuanzia propaganda hadi kufikia mbinu za kisayansi, na mtutu wa bunduki !

Je kweli ndugu yangu muislamu mpaka hapo bado tunataraji kupata msaada wa mtu mwingine asiye kuwa muislamu aje atutibu maradhi yetu?

Bila shaka sote tutasema;Laa.

Basi haraka ndugu yangu tutafute tiba wenyewe. Na kwa sababu maradhi yenyewe ni ya dini, basi hakuna budi isipokuwa kuyarudisha kwenye vipimo vya dini, Qur’an na Hadithi za Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kwasababu maradhi hayo hayapimwi kwa kutumia x ray, wala Ultrasound scan..

Na siyo kila anayeitwa Daktari anao uwezo wa kuyatibu maradhi hayo, bali hakuna budi kumrejea Daktari muhusika (Specialist) wa maradhi haya.
Natunapo mrejea Daktari bingwa wa maradhi ya Umma huu, ambaye ni Sayyidna Muhammad Ibin Abdillahi -swalla llaahu alayhi wasallam- tunamkuta ameshatuelezea maradhi yote, kuanzia sababu zake, athari zake, na tiba zake, mpaka namna ya kujikinga, na kuchukua tahadhari na maradhi hayo.

Hebu sasa ndugu yangu Muislamu tuingie kwenye maabara ya Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- ili tuanze uchunguzi wa kina juu ya maradhi yetu haya yanayo tudhoofisha, bila shaka tukifanya hivyo tutaigundua tiba yetu.

Na hatua ya kwanza kabisa ya uzima wetu ni kukubaliana na matokeo ya uchunguzi huo.

Amesema Allah {ﷻ}:
وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْراً أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالاً مُّبِيناً {الأحزاب36

“Haiwi kwa muumini mwana mume, wala muumini mwanamke, atakapo hukumu mwenyezi Mungu na Mtume wake jambo lolote, kuwa na hiari katika shauri lao..”.
Aya ya 36 Sura ya33.

Kwa hiyo tunalazimika kukubali matokeo,Je Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- anatueleza nini juu ya maradhi yetu? Kwa kifupi tunaumwa nini?

Hebu tuanze na hii Hadithi tukufu ya Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-:

- Siku moja Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- alipanda juu ya mimbari yake tukufu akawapa mawaidha watu mpaka wakalia sana, na wakadhani kwamba mawaidha hayo ni ya kuwaaga, wakamwambia Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-: tuusie.

Akasema Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- akasema:

“Ninakuusieni ucha Mungu, na kuwa wasikivu, na watiifu, hata kama aliye watawala ni mtumwa wa kihabeshi,
kwa sababu atakayeishi baada yangu miongoni mwenu ataziona IKH’TILAFU NYINGI, basi nyinyi LAZIMIANENI NA SUNNA ZANGU, na Sunna za Makhalifa wangu waongofu wenye kuongoka, ziumeni Sunna hizo kwa magego, NA TAHADHARINI NA UZUSHI wa mambo, kwani kila lenye kuzuliwa ni bid’a, na kila bid’a ni upotevu, na kila upotevu ni motoni.”

Wameipokea Hadithi hii maimamu hawa;
Abu Daud, Tir'midhi, Ibin Majah, Ah'mad, na Hakim, na wengineo.

Baada ya kukubaliana kwamba tuna maradhi,na wengi wetu hatujui tunaumwa nini, tumemrejea Daktari wetu bingwa Sayyidna Muhammad -swalla llaahu alayhi wasallam- ripoti anayotupa ni kwamba;

-Sisi tuna maradhi makubwa sana, maradhi hayo jina lake ni (BID’A) UZUSHI katika dini.

- Na katika alama kuu za maradhi haya ni hizi ikh’tilafu na tofauti zetu zisizo kwisha.

- Dawa yetu sisi si mzizi wala si hirizi, bali ni kushikamana na mafundisho yake Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- na mafundisho ya Makhalifa wake waongofu.

- Na kinga yetu ni kujiepusha na Uzushi katika dini, kuzusha mambo ambayo hatukufundishwa na Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-

- Na madhara ya maradhi haya hayaishilii katika hizi tofauti zetu tulizo nazo, bali maradhi haya yatatuangamiza mpaka kutuingiza motoni -Allah atukinge na moto wake- Aamiin.

Kwa ufupi haya ndiyo matokeo yetu baada ya uchunguzi uliofanyika katika maabara ya Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam-.

Je ndugu muislamu unayakubali matokeo haya ambayo yanatoka katika maabara ya Bwana Mtume {s.a.w.}?

Hebu ikumbuke aya ya36 ya sura ya 33.

Kwahiyo mpaka hapa tumegundua kwamba;

BID'A (UZUSHI) katika dini ni miongoni mwa maradhi mabaya yanayo tudhoofisha sisi waislamu,bali ndiyo chemchem ya mizozo yetu.

Ukiwa ndugu yangu muislamu umeyafahamu matokeo na kuyakubali labda sasa utapenda kujua zaidi ni nini maana sahihi ya bid'a (Uzushi) katika dini?

## NI NINI MAANA SAHIHI YA BID'A (UZUSHI)?

Jawabu ni kwamba,maana sahihi ya (Bid'a) Uzushi katika lugha ya kiarabu ni;

هي كل شئ مخترع على غير مثال سابق

"Ni kila jambo lililo zushwa pasi na kuwa na mfano uliotangulia".

Ama Bid'a (Uzushi) katika sheria ya kiislamu, ni kama alivyosema Imamu As shatwiby;

.يقصد بالسلوك عليها المبالغة فى التعبدلله سبحانه,هي طريقة فى الدين مخترعة تضاهي الشرعية

"Bid'a ni njia (utaratibu au mfumo) uliozushwa katika dini ambao unafanana na utaratibu wa kisheria, uliokusudiwa kwa kuufuata utaratibu huo kupituka mipaka katika kumuabudu Allah -Sub'haanahu wata'alaa-.
tazama al I'tiswaam 1/37.

Ufafanuzi wa maneno haya;

-Kwa mujibu wa maelezo haya ya bidaa ni kwamba, kuzusha utaratibu au mfumo -katika ibada- ambao ukiutazama kwa dhahiri unafanana na utaratibu wa kisheria na hali ya kuwa sheria haikuuweka utaratibu huo katika ibada hiyo, kufanya hivyo ni bidaa.

Kama vile kujiwekea mitindo maalumu ya ibada bila ya idhini ya sheria kwa makusudio ya kuzidisha katika kumuabudu Allah kwa dhana ya kwamba utaratibu uliowekwa na sheria hautoshi, mfano ni kama ile mitindo ya kizushi iliyowekwa katika ibada za kumdhikiri Allah, na kumswalia Bwana Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- kuzusha mitindo kama hiyo ni bid'a, na ibada hizo kwa mifumo hiyo iliyozushwa haitokubaliwa na sheria.

Na alipo kuwa akiiweka wazi zaidi maana ya bidaa, sheikh huyo akaelezea kwamba bidaa ziko kwenye sehemu tatu;

1- البدعة الحقيقية bidaa ya kiuhakika.

nayo ni ile bidaa ambayo haina dalili yoyote ya kisheria, si katika asili yake, wala katika mtindo na mchanganuo wake.

2- البدعة الاضافية bidaa kwa nisba maalumu.

Nayo ni ile ambayo ina ncha mbili;

a) Ncha moja ukiitazama iko katika sheria.

b) Ncha nyingine haiko katika sheria.

Kwa sababu ibada yoyote ile ina ncha mbili, kwanza ni ibada yenyewe, pili ni utaratibu na mfumo wa ibada hiyo,na ama zile ibada ambazo hazikuwekewa utaratibu na mfumo maalumu, huko kutokuwa na utaratibu na mfumo, huo ndiyo utaratibu na mfumo wenyewe, na haitofaa kuubadilisha utaratibu na mfumo huo, na kufanya hivyo ni bidaa.

Hapa tutatoa mifano mitatu miongoni mwa mifano mingi.
Mfano wa kwanza;

Kuna swala inayoitwa Swalatur-Raghaaibi nayo ni swala ambayo huswaliwa rakaa kumi na mbili katika kila usiku wa ijumaa ya mwanzo ya mwezi wa Rajab na mwezi wa shaabani kwa utaratibu na mtindo maalumu ambao haukuwekwa na sheria.

Lakini ukiiangalia ncha moja utaiona imeegemea kwenye sheria, yaani kwa ufupi ni kwamba ukiiangalia utaiona kuwa ni swala, na swala kisheria ni kitu bora kilichohimizwa.

Lakini ukiitazama ncha ya pili utaiona kwamba haikuegemea katika sheria, yaani utaratibu na mtindo wa swala hiyo haukufundishwa na sheria, bali umezushwa.
Na ndiyo maana maulamaa wote walipoulizwa kuhusu hukumu ya swala hiyo, wakajibu kwamba swala hiyo ni bidaa, miongoni mwa maulamaa hao ni Imamu An-nawawy alipoulizwa nini hukumu ya swala hiyo? alijibu hivi:

بدعتان موضوعتان منكرتان قبيحتان

"Swala-hizo za Rajab na Shaabani - ni bid'a mbili zilizozushwa, zilizo ovu, tena mbaya".
Tazama It'hafus sadatil muttaqina 3/424.

Je unajua kwanini Imamu An nawawy anatwambia kwamba kuswali swala hii ni uzushi?

Je kwasababu swala hii haina asili katika dini? au ni kwasababu ya mfumo wake huu haukufndishwa na sheria?

Na ufahamu kwamba huyu ni mwanawachuoni mkubwa katika madhehebu ya kishaafy, na wala si WAHABI!!

Mfano wa pili;

Ni kumswalia Mtume -swalla llaahu alayhi wasallam- baada ya adhana au wakati wa Iqaama ya swala kwa sauti ya juu, kwa kiasi ambacho inafahamisha kwamba kufanya hivyo ni sehemu katika adhana au Iqaama.

Ukiitazama asili ya kitendo hicho cha kumswalia Mtume {s.a.w.} utakiona kuwa kimo katika sheria,lakini ukiutazama mtindo ambao unatumika hapo utauona kwamba haukufundishwa na sheria.

Na ndiyo maana alipo ulizwa Imamu Ibin Hajar al Haytamy kuhusu kumswalia Mtume{s.a.w.} baada ya adhana kwa mtindo huo tulioutaja akasema hivi;

الأصل سنة والكيفية بدعة

[Asili ni sunna,na mtindo ni bidaa].

Tazama al fatawa al Hadithiyatil kub'ra,1/131.

Na huyu naye pia ni katika maulamaa wakubwa wa kishaafy anatwambia kwamba kumswalia Mtume{s.a.w.} kwa mtindo na utaratibu huu ni bidaa !! na yeye bila shaka si wahabi.

Mfano wa tatu;

ni kuleta dhikiri (Laa ilaha illa llahu) kwa kunyanyua sauti wakati wa kwenda kuzika.

Ukiitazama asili ya kitendo hiki cha dhik'ri utakikuta kwamba ni jambo ambalo limo ndani ya sheria.

lakini ukiutazama mtindo huu unaotumika utauona kwamba haukufundishwa na sheria bali ni mtindo wa kizushi.

amesema Imamu An nawawy kuhusu kulifanya jambo hili kwa mtindo huu;

**واعلم أن الصواب المختارما كان عليه السلف رضي الله عنهم السكوت حال السير مع الجنازة فلا يرفع صوت بقراءة ولا ذكر ولا غير ذللك.**
**فهذا هو الحق ولا تغترن بكثرة من يخالفه...**

[Fahamu kwamba jambo ambalo ni la sawa sawa lililo chaguliwa ni ile hali waliyo kuwa nayo salaf (maswahba na waliowafuatia kwa wema) ni hali ya ukimya wakati wa kwenda na jeneza,na hainyanyuliwi sauti kwa kisomo wala dhikri wala jambo jingine…na kufanya hivi ndiyo haki,wala usihadaike na wingi wa wenye kuhalifu] !!

Tazama kitabuchake  Al adh'kaar,ukurasa 157.

Kwahiyo ujue ndugu muislamu kwamba kwenda na jeneza huku watu wanapiga kelele wakidai kwamba ni dhikiri,jambo hilo si haki bali ni batili. Na anayesema maneno  hayo ni mwanawachuoni mkubwa wa kishaafy!

Je ndugu yangu kwa mujibu wa fatawa hizo za maulamaa wakubwa wa kishaafy tulizozitaja katika mifano hiyo mitatu Je unataka kuniambia kwamba maulamaa hawa wanawakataza watu kuswali?

Au unataka kuniambia kwamba wanawakataza watu kumswalia Mtume {s.a.w.}? na je wanawakataza watu wasifanye dhik'ri?
Bila shaka jawabu litakuwa ni La.

Je maulamaa hawa wanakataza nini? Ukiwa ni katika wale wanao yatazama mambo kwa makini na mazingatio,bila ya kutanguliza matamanio ya nafsi mbele utasema kwamba wanacho kikataza maulamaa hawa ndicho kile kile kincho katazwa na Answaaru Sunnah,nacho ni kuzusha katika ibada taratibu na mifumo ambayo haikufundishwa na Mtume {s.a.w.} jambo ambalo halifai katika uislamu.

Kwasababu haifai katika uislamu kubuni na kuzusha taratibu na mifumo za ibada yoyote ile bila ya kupata idhini ya sheria.

Kwa hivyo basi,siyo insafu wala si uadilifu kabisa kwa ndugu zetu watetezi wa mambo ya uzushi,kama vile mikusanyiko ya maulidi na mingineyo, wanapokuwa wanakatazwa kuzusha mitindo hiyo,wao mbio hukimbilia kusema kwamba hawa wanawakataza watu kumswalia Mtume{s.a.w.} !!

Hivi kweli kuna muislamu wa kweli hasa,anaye muamini Mwenyezi Mungu na Mtume{s.a.w.} na kuamini siku ya malipo halafu anapinga kumswalia Mtume{s.a.w.}?

Au hizo ni mbinu za kutaka kuendelea kuwatia watu michanga ya macho?!

3- البدعة التركية bidaa ya kuacha;

Nayo ni kuifanya ibada yoyote ile ambayo hakuifanya Bwana Mtume{s.a.w.} wala hakuifundisha,na hali ya kuwa sababu za kuifanya zilikuweko,na hakukua na vizuizi vya kumzuia,na hii ina mifano mingi sana hapa chini tutaitaja mifano mitano;

**1-ni kuadhini katika swala za eid;**

Mtume{s.a.w.} ameswali eid nyingi katika uhai wake,lakini hakukuwa kukiadhiniwa kwa ajili ya swala hizo hata mara moja,kuishiria kwamba kuadhini katika swala hizo si katika uislamu,na kama ni katika uislamu angefundisha Bwana Mtume{s.a.w.}.

**2-Kuleta Tak'bira wakati wa kuzika;**

Mtume{s.a.w.} amewazika watoto wake,wake zake na ndugu,pamoja na maswahaba zake,lakini hajawahi kulifanya hilo,kuishiria kwamba kufanya hivyo siyo uislamu,na lau kama lingekuwa jambo hilo ni katika uislamu angelifundisha.

**3- Kuleta dua na nyiradi za pamoja kwa sauti baada ya swala;**

Bwana Mtume{s.a.w.} amewahimiza na kuwasisitiza watu wamuige swala yake,na pia amewasisitiza watu waswali kama alivyokuwa akiswali,
Na katika swala yake {s.a.w.} hakuna suala la kuleta nyiradi kwa pamoja, si kabla ya kuswali wala baada yake,na lau kwamba jambo hilo nalo lingekuwa ni dini bila shaka angelifundisha.

4-Na hali kadhalika mikusanyiko ya maulidi,nayo pia Mtume {s.a.w.} hakuifanya,wala hakuifundisha,na lau kwamba ingekuwa ni dini angelifundisha jambo hilo,lakini muda wa kuwa hakulifundisha basi ujue kwamba jambo hilo siyo dini.

5- Mikusanyiko ya dhik'ri za vikohozi,mikusanyiko hii na mitindo hii ni mipya katika uislamu,na lau kama ingekuwa ni dini basi pia angeifundisha Sayyid'na Muhammad {s.a.w.}.

Sasa hebu tuwaulize ndugu zetu hawa wanaotetea uzushi wa maulidi maswali yafuatayo;

-sote tunafahamu kwamba kumswalia Mtume{s.a.w.} ni katika ibada zenye fadhila nyingi mno katika uislamu,swali;

je ibada hii imewekewa utaratibu maalumu au la?

Na kama jawabu itakuwa ni naam, je kwanini hamuufuati utaratibu huo uliowekwa na sheria?

Au mnataka kutuambia kwamba utaratibu huo ni pungufu kwahiyo mnataka kuutimiza nyinyi?

Na kama jawabu ni la,

Je ninani aliyekupeni  idhini na kibali cha sheria cha kuweka na kuzusha mitindo ya ibada katika dini?

au mnadhana ya kwamba kumswalia Mtume{s.a.w.} na kumuadhimisha siyo katika ibada kwahiyo kila mtu yuko huru kujifanyia anavyo taka?

Kama mnadhana hii basi mjue kwamba mmekula hasara duniani na akhera. Ikiwa hamna kibali hicho cha kisheria,basi hamjui kwamba kuzusha katika dini mambo ambayo hayamo ni haramu? Na kwamba hiyo ibada yenu ya kizushi haitokubaliwa?!

Je hamuoni kwamba mnaingilia kazi ambazo si zenu? basi jiandaeni na kuulizwa mbele ya Allah {s.w.t.}.

Hata kama mtadai kwamba eti nia zenu ni nzuri katika kuufanya uzushi huu na mwengineo,nia zenu nzuri hazito saidia kitu,
kwasababu kuwa na nia nzuri pekeyake katika kufanya ibada haitoshi, mpaka nia nzuri hiyo iambatane na kuufuata utaratibu alio ufundisha Bwana Mtume{s.a.w.} katika kuitekeleza ibada hiyo.

Bila shaka ndugu muislamu utakuwa umefahamu nini maana sahihi ya bidaa.

Kwa ziada nitapenda uyajue mambo haya yafuatayo kwani ni muhimu sana,na yatakusaidia zaidi katika kuijua bidaa,na kuepukana na usumbufu wa wababaishaji;

-Ndugu muislamu,fahamu kwamba jambo lolote ambalo amelifundisha Bwana Mtume{s.a.w.} ima kwa kauli yake,au kwa kitendo chake,au kwa kuwa limefanyika mbele yake,naye akalikubali,basi jambo hilo ni Sunna,na siyo bidaa.

Kwahiyo usikubali kupewa mifano ya kufaa kuzusha katika dini kwa vitendo vya maswahaba walivyo vifanya mbele ya Mtume{s.a.w.} naye{s.a.w.} akavikubali.

-Fahamu pia kwamba jambo lolote ambalo hakulifanya Bwana Mtume{s.a.w.} kwa kukosekana sababu ya kulifanya jambo hilo,ikipatikana sababu baada ya kuondoka Mtume {s.a.w.} kulifanya jambo hilo baada yake ni sunna,na siyo bidaa,kama vile kuikusanya Qur'an katika msahafu mmoja.

-Pia ufahamu kwamba jambo lolote ambalo hakulifanya Bwana Mtume{s.a.w.} kwa kwasababu ya kupatikana vizuizi vilivyo mzuia,kulifanya jambo hilo baada ya kuondoka vizuizi hivyo,ni sunna na siyo bidaa,kama kudumu kuswali swala ya tarawehe kwa jamaa.

-Pia ufahamu kwamba jambo lolote ambalo si la ibada,kama kupanda ndege, magari,au kutumia computer,Ac,mafeni,mabusati,meza,viti,n.k,kuvitumia vitu hivi si bidaa, kwasababu bidaa inaingia katika mambo ya dini tu.

Kwahivyo basi,ile hadithi ya Mtume{s.a.w.} tuliyoitaja hapo nyuma kwenye utangulizi,hadithi hii inaenea bidaa zote katika dini,kwasababu neno lililo tumika hapo ni neno la kiarabu كل"KULLU"ambalo asili yake linaenea kila kitu kilichotegemezwa baada yake,bila ya kutoka chochote mpaka kwa dalili.

Na kuna mifano mingi ya matumizi ya neno hilo kwa maana tuliyoitaja, na miongoni mwa mifano hiyo ni kauli ya Allah{ﷻ} pale aliposema;.

الأنبياء35{كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ }

[kila nafsi ni yenye kuonja mauti..]
suratul Anbiyaa (21)aya35.

Hapo limetumika neno kullu kama lilivyo katika asili yake,kwahiyo linafahamisha kwamba viumbe vyote vilivyo na nafsi vitakufa,na hakuna kitakacho ishi milele,
na vivyo hivyo ndivyo lilivyo tumika neno hilo katika hadithi hii ya Bwana Mtume{s.a.w.} aliposema;

"وكل ضلالة فى النار,وكل بدعة ضلالة ,اياكم ومحدثات الأمور فان كل محدثة بدعة.."

[..tahadharini na mambo ya uzushi,kwasababu kila lenye kuzushwa ni bidaa,na kila bidaa ni upotevu,na kila upotevu ni motoni].

Kwa hiyo hadithi hii itaenea kila jambo la bidaa kwa maana tuliyoitaja,kwahiyo hadithi itafahamisha kwamba kuzusha jambo lolote katika dini ni bidaa,na halito kubaliwa,na sababu iliyopelekea kusema hivyo,ni hilo neno lililotumika hapo ambalo ni kullu.

Lakini kwa bahati mbaya baadhi ya ndugu zetu wanaotetea mambo ya uzushi katika dini wao hawaikubali maana hii,wao wanasema kwamba hili neno kullu hapa halikuenea kila kitu,kwa maana ya kwamba limetumika nje ya maana yake ya asili,kama lilivyo tumika neno hili katika aya ya 79 ya suratul Kah'fi,amesema Alla{ﷻ};

79الكهف{وَكَانَ وَرَاءهُم مَّلِكٌ يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ غَصْباً }

[..Na alikuweko mbele yao mfalme anaye lichukua kila jahazi kwa kulipora].

Ndugu zetu hawa wanaotetea mazushi katika dini wanapoitoa aya hii kwa kawaida husema hivi;

Hapa katika aya hii limetumika neno kullu,lakini halikuenea kila kitu,kwanini?

Naam,lau kama huyu mfalme angekuwa anachukua kila jahazi,lililo zuri na baya kusingekuwa na faida yoyote kwa al Khidh'ri {a.s.} kulivunja lile jahazi la masikini,kwahiyo inaonyesha kwamba mfalme huyu anachukua majahazi mazuri tu.

Pamoja na kwamba limetumika neno kullu katika aya hii,lakini neno hilo halikuenea mpaka majahazi mabaya,na ndiyo sababu ya al khidh'ri {a.s.} kulivunja lile jahazi la masikini,ili liwe baya,na hatima yake halito porwa na mfalme,hivyo basi kullu haienei kila kitu,na kama inaenea ingeenea hapa,hivyo basi haitofaa kuitumia hadithi hii isemayo;

[..fainna kulla bid'atin dhalaalah..] [..hakika kila bidaa ni upotevu..] Kupingia maulidi,kwasababu neno'kullu' lililo tumika hapo halikuenea,kama vile ambavyo halikuenea katika aya tuliyoitaja,hivyo basi,siyo kila uzushi ni upotevu,bali kuna uzushi mwingine katika dini ni mzuri!

Hebu hapa tuwaelimishe kidogo;

Sisi tunasema kwamba asili ya neno kullu linapotumika linaenea kila kitu,na ushahidi ni aya tuliyo itoa isemayo;

[kila nafsi niyenye kuonja mauti].

Lakini pamoja na hivyo neno hilo linaweza kutumika nje ya maana yake ya asili,pale itakapo patikana dalili ima ya kisheria au ya kiakili itakayo fahamisha hivyo,kwenye aya wanayoitumia kuna dalili ya kiakili ambayo inafahamisha kwamba kullu hapo imetumika nje ya eneo lake la asili,na si asili yake kutumika hivyo.

Kwahiyo haitofaa kuifananiza kila kullu inayotumika katika maneno ya kisheria na kullu hiyo iliyotumika katika aya hiyo,bali sahihi ni kulitumia neno hilo kama lilivyo katika asili yake ambayo ni kuenea kila kitu,kama ilivyo katika aya hii ya mauti.

Hebu ndugu msomaji tuitazame vizuri hadithi hii ya Bwana Mtume{s.a.w.} pamoja na kulizingatia hili neno kullu lililo tumika hapo,
hebu itazame hadithi hii kwa makini kabisa, hebu rudia tena na tena,kisha zihesabu kullu zilizo tumika hapo,ukifanya hivyo utagundua kwamba ndugu zetu hawa ni wababaishaji,na hawana hoja za kielimu zaidi ya ubabaishaji kwanini?

Naam, labda baada ya kukariri kuitazama hadithi hii,na kuzihesabu kullu zilizo tumika katika kipande hicho cha hadithi hii ndefu
bila shaka umegundua kwamba kullu hapa ziko tatu;

1-..fa inna <u>kulla</u> muh'dathatin bid'ah.[hakika kila lenye kuzushwa ni bidaa].

2-wa <u>kulla</u> bid'atin dhalaalah.[na kila bidaa ni upotevu].

3-wa <u>kulla</u> dhalaatin fin naar.[na kila upotevu ni motoni].

Sasa hebu ndugu msomaji,tujaribu kuhoji taratibu kama ifuatavyo;

Je,kuna tafauti gani kati ya kullu hizi zilizotumika hapa?
bila shaka jawabu litakuwa hakuna tafauti hata moja.
Na kama hakuna tafauti yoyote;

Je,kullu zote hizo hazienei? na kama ziko zinazoenea kwanini zienee na nyingine zisienee?

Wanaoitumia hadithi hii,kupambana na uzushi katika dini(Answaaru sunna) wanasema;

Kullu zote hizo zinaenea na zimetumika katika asili yake,kwahiyo hakuna uzushi mzuri katika dini,bali kila uzushi katika dini ni upotevu,na kila upotevu ni motoni.

Wanaotetea mambo ya uzushi katika dini wanasema;

Kullu zote hizo hazikuenea,kama vile ambavyo haikuenea kullu ile iliyo tumika katika aya ya jahazi la masikini,
kwahiyo siyo kila uzushi katika dini haufai,bali upo uzushi mzuri katika dini.

Wanaosema kwamba kullu hapa imetumika katika asili,kwahiyo imeenea,wanawauliza wale wanaosema kwamba kullu hapa haikuenea swali lifuatalo;

Ikiwa kullu zote hizi hazikuenea kama mnavyodai,na kwasababu hiyo mnasema kwamba kuna uzushi mzuri katika dini, kwamaana ya kwamba mtendaji wa uzushi huo atakuwa ametenda jambo zuri,na kustahiki kupewa thawabu!

Sasa je katika dini kuna upotevu ambao ni mzuri ?

Kwa maana ya kwamba je kuna upotevu ambao mtendaji wa upotevu huo atastahiki kuingia peponi kwasababu yakutenda upotevu wake huo? kwasababu hapo pia limetumika neno kullu ambalo kwenu nyinyi halienei kama mnavyodai!

[..wakulla dhalaalatin fin naari..] [na kila upotevu ni motoni..]

Kwasababu huyo aliyesema kila bidaa ni upotevu,ndiye huyohuyo,tena hapohapo aliyesema;

[..na kila upotevu ni motoni..]!

Tena kwa kuitumia kullu hiyo hiyo.
Na kama hapa-kwenye upotevu- imeenea,kwanini pale-kwenye bidaa-isienee? tunaomba jawabu ya kielimu.

Kwa ufupi ni kwamba hii Kullu iliyokuja hapa katika hadithi hii imeenea kila kitu kama ilivyo katika asili yake,na kila lililozushwa katika dini ni Bidaa,na kila bidaa ni upotevu, kama vile ambavyo kila upotevu unapelekea motoni.

Pengine labda utauliza kwamba;kwanini mmeihusisha bidaa isiyofaa katika dini tu?

Jawabu ni kwamba;

Tumehusisha bidaa katika dini tu kwasababu ya hadithi nyingine ya mtume{s.a.w.} ambayo inaiweka wazi zaidi hadithi hii,pale aliposema{s.a.w.};

"من أحدث فى أمرنا هذا ما ليس منه فهو رد"

[mwenye kuzusha katika dini yetu hii jambo lisilo kuwemo,basi jambo hilo ni lenye kurudishwa],halito kubaliwa.

Kwahiyo pale Mtume {s.a.w.} alipo zungumzia uzushi, makusudio yake yalikuwa ni uzushi katika dini,na siyo katika mambo ya kidunia,kwahiyo tanababhi wasije wakakupa mifano ya magari,na pikipiki, n.k,maana hao ni wababaishaji.

Na ama hapa mtume{ﷺ} aliposema;

[Mwenyekuzusha..jambo lisilo kuwemo..].

Ana maanisha kwamba kuzusha jambo lisilo kuwemo katika dini,ima asili ya jambo,au utaratibu na mfumo wake,au idadi,au wakati,au mahali,basi uzushi huo hautokubaliwa,na atarudishiwa mwenyewe uzushi wake huo, hata kama atadai kwamba nia yake katika kuzusha uzushi huo ni nzuri.

kwasababu amali yoyote ya mtu haito kubaliwa mpaka yakamilike masharti makuu mawili;
1-ikh'lasi -nia njema kwa ajili ya mwenyezi mungu peke yake-.

2-kuafikiana na sunna-kuitekeleza amali hiyo kwa utaratibu alio ufundisha Bwana Mtume{s.a.w.}-.

Na ikikosekana moja ya masharti haya,basi amali yoyote ile,ya mtu yoyote yule,popote alipo,na vyovyote awavyo,amali yake hiyo haitokubaliwa,na atarudishiwa mwenyewe,kwahiyo unapotenda ibada yoyote kwanza kabisa chunga sana ikhlasi,kisha jiulize;

Je hivi ninavyo fanya ndivyo alivyofundisha mjumbe mtukufu wa mwenyezi mungu Muhammad bin Abdillahi{s.a.w.}?
Kama hivyo unavyo fanya sivyo alivyofundisha Bwana huyo basi ujue hakuna rai katika dini,kwahiyo wacha jambo hilo hata kama una nia njema, nia njema hiyo haito kusaidia kitu mbele ya Allah{s.w.t.} na hiyo ndiyo maana ya MuhammadunRasuulullahi.

-kwa mfano kuzusha sheria tafauti na sheria ya Mwenyezi mungu,uzushi huo hautokubaliwa.

-au kuweka mfumo maalumu katika kumdhikiri mwenyezi mungu,au kumswalia mtume{s.a.w.} mfumo,na utaratibu ambao haukufundishwa katika dini,utaratibu,na mfumo huo hauto kubaliwa.

-Au kuweka idadi ima ya rakaa au tawafu kwenye kaaba au sa'ai baina ya swafaa na mar'wa idadi ambazo hazikufundishwa katika dini,idadi hizo hazito kubaliwa.

-Au kuweka siku,au wakati maalumu kwa ajili ya ibada,na hali ya kuwa sheria haikuweka wakati maalumu kwa ajili ya ibada hiyo,kama kuihuisha siku ya tarehe 12 ya mwezi wa mfungo sita na nyinginezo,kwa ajili ya kusherehekea mazazi ya mtume{s.a.w.} na kumswalia,sheria ya kiislamu haikufundisha jambo hilo,kwahiyo jambo hilo halitokubaliwa,na atarudishiwa mwenyewe mzushi uzushi wake huo,hata kama wazushi watadai kwamba nia zao ni njema.

-Vilevile kuhusisha mahali maalumu kwa ajili ya ibada,na ukaitakidi kwamba kufanya ibada mahali hapo ni bora,na hali ya kuwa sheria haija fundisha hivyo,kama kuitakidi ubora wa kufanya ibada katika ardhi ya Kar'bala,au kutufu kwenye makaburi,na kuswali kwenye eneo la makaburi kwa kuitakidi kupata baraka-hayo ni katika mambo yanayopelekea kwenye shirki-na ibada hiyo haito kubaliwa na itarudishwa kwa mwenyewe mzushi.

Huwenda baadhi ya watu wanaweza kuhoji kwa njia ya kutaka kuwababaisha wasiosoma,kwa kusema kwamba Mtume {s.a.w.} katika hadithi hii amesema;

[mwenye kuzusha…jambo lisilo kuwemo...].

Je kuzusha jambo lililo kuwemo litakubaliwa?

Jawabu ni kama ifuatavyo;
Kwa lugha ya kitaalamu,watu wa usulul fiq'hi,wanaiita sentensi hiyo (jambo lisilo kuwemo) kuwa ni صفة كاشفة' swifatun kaashifah'
kwahiyo haina kinyume,kwa maana ya kwamba jambo lolote lililozushwa katika dini ni kwamba halimo,na lisilo kuwemo ni lile lililozushwa.

Na mfano wake katika Qur'an ni ile aya isemayo;

..إِنَّا أَنزَلْنَا التَّوْرَاةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُواْ }
المائدة44

[Hakika sisi tumeiteremsha Taurati mna ndani yake uongofu na nuru,wanahukumu kwayo Manabii ambao wamesilimu...]
Suratul maidah aya 44.

Hicho kipande tulicho kipigia mstari maulamaa wanakiita **'swifatun kaashifah'**kwahiyo hakina kinyume,hivyo basi, huwezi kusema kwamba eti kuna manabii ambao si waislamu kwa kutegemea kinyume cha aya hiyo,kwasababu manabii wote wamesilimu /waislamu.

Hebu turudi katika hadithi yetu,tunasema hivi;huwezi kufanya jambo ambalo halimo halafu likawa si uzushi,na wala huwezi kufanya jambo ambalo ni uzushi kisha likawa limo katika dini.

Tanabahi ndugu yangu haya ni mas'ala ya kielimu! mara nyingi mas'ala haya huwekwa wazi na mifano hai.

Labda sasa tumalizie makala yetu hii ya leo kwa kuyaweka wazi mas'ala haya kwa kukitaja kisa sahihi tena mashuhuri, kilicho tajwa na maulamaa wakubwa wa Hadithi na Historia ya kiislamu,kama vile imamu Addaarimy kwenye sunan yake,na Imamu Abu Nuaim kwenye Hil'ytul awliyaa,na Imamu Bah'shal katika Tarekh waasit;

kutoka kwa Amru bin Salamah mwanafunzi wa swahaba mkubwa Abdullahi bin masoud{r.a.} anasimulia kwamba;

[siku moja Abdillahi bin Masoud,na Abu mussa Al Ash'ary walitoka nyumbani kwa Ibin masoud kwenda msikitini, walipofika msikitini waliwakuta watu wamekaa vikundi mduara wanamdhikiri Allah na mikononi mwao wana mawe ya kuhesabia dhikri zao,na katika kila kikundi kuna mtu mmoja anaye sema;
semeni 'ALLAHU AK'BARU'mara mia moja,nao wanasema kwa mara hizo.
Semeni 'LAAILAHA ILLA LLAHU' mara mia moja.nao husema kwa mara hizo.
Semeni 'SUB'HAANA LLAHI' mara mia moja,nao wanasema kama walivyoamriwa.
Ibin Masoud{r.a.} akawaendea mpaka karibu,kisha akawauliza; mnafanya nini? wakajibu haya ni mawe tunahesabia Takbira,Tah'lili,na Tas'bihi.
Akasema Ibin Masoud;
Mmeangamia nyinyi!!

Enyi umma wa Muhammad ni haraka ilioje hii ya kuangamia kwenu!

Hawa ni maswahaba wa mtume wenu bado wako wengi,na hizi ni nguo zake{s.a.w.} bado hazija chakaa,na hivi ni vyombo vyake bado havija vunjika,naapa kwa mwenyezi mungu ambaye nafsi yangu iko katika mikono yake,itakuwa nyinyi mko katika mila nzuri zaidi kuliko mila ya Muhammad,au mtakuwa nyinyi mnaufungua mlango wa upotevu, wakasema Ee Abaa Abdil rah'man!

Sisi hatukukusudia isipokuwa kufanya kheri Ibin Masoud akawaambia; kwani kuna watu wangapi wanakusudia kufanya kheri lakini hawaipati? Kisha akaamrisha watolewe msikitini].

Hebu tuanze kuhoji;

-kwa mujibu wa kisa hiki sahihi, je maswahaba watakuwa wameelewa kwamba kuna bidaa nzuri,   kama walivyoelewa watetezi wa Uzushi wa zama za leo?

Au wameelewa kwamba kila uzushi ni upotevu kama walivyoelewa watetezi wa Sunna za Mtume{s.a.w.}?

-Kama kuna uzushi mzuri katika dini,kwanini Ibin Masoud awaambie hawa walio kusanyika msikitini kwa ajili ya kumdhikiri Allah kwa mfumo na utaratibu ambao haukufundishwa na mtume{s.a.w.} kwamba wanafungua mlango wa upotevu?

-Je lau kama Ibin Masoud angefufuka leo hii na kuwakuta hawa watu wa zama za leo wanaofanya hizo zinazoitwa dhikiri kwa vikohozi na kupandisha pepo! Wanawake kwa wanaume,na wakapewa na vyano,na tasbihi za kuburutika, je angewawacha?bila shaka jawabu unalo.

-Hivi ndugu yangu muislamu,lau kama Swahaba huyu,atakuja katika zama hizi zetu akawakuta watu katika hadhara zao za dhikiri,au maulidi kisha akawaambia maneno kama haya aliyo waambia wazushi wa zama zake,hivi kweli wanajazba watambakisha?Au bakora zitavuma,na atolewe yeye msikitini? Na kuambiwa kwamba Ibin Masoud ni WAHAB! Hataki dhikri,na hampendi Mtume{s.a.w.}?!

-Je kwanini hao walio katazwa na Ibin Masoud{r.a.} wasimkumbushe Ibin Masoud aya na hadithi za ubora wa kumdhikiri mwenyezi mungu,na hadithi zinazoonyesha kufaa kwa kuzusha mambo mazuri?

Kama wao hawazijui, je Ibin Masoud,na maswahaba wenzake aliokuwa nao,na wanafunzi wao hawazijui aya na hadithi hizo?
au wanazijua,lakini wanajua kwamba aya na hadithi hizo hazitumiki mahali hapo?

-lakini kwabahati mbaya zaidi,hii leo mtu mbaya,na mkorofi zaidi ni yule atakaye simama kupinga uzushi,ataambiwa anatukana watu! hana hekima! hajui kufikisha ujumbe! hana elimu! anataka kuleta far'ka! Kwani kasoma wapi huyo? huyo ni Wahabi hampendi mtume{s.a.w.}! na maneno chungu nzima ya kizushi.

lakini leo hii wako wapi watu kama kina Abdillahi bin Masoud waliofahamu kwamba miongoni mwa matatizo yanayo udhoofisha umma ni gonjwa kuu la uzushi??!

Ibin Masoud huyu,ndiye yule ambaye Sayyidna Muhammad{s.a.w.}amesema;

[yule ambaye anataka kuisoma Qur'an kama ilivyoteremka-kutoka mbinguni-basi na aisome kwa kisomo cha mtoto wa mama Abdi] na mtoto wa mama Abdi ni Abdillahi bin Masoud{r.a.}.

Na yeye ndiye aliyemliza Sayyidna Muhammad kwa kisomo chake,pale Bwana Mtume{s.a.w.} alipomwambia;Nisomee Qur'an,Ibin Masoud akamwambia; nikusomee wewe nahali Qur'an imeteremshwa kwako?

Mtume{s.a.w.} akamwambia; nami napenda kuisikia kwa mtu mwingine, Ibin Masoud{r.a.} akaanza kuisoma sura ya 4 An nisaa, mpaka alipoifikia Aya ya 41,Bwana Mtume{s.a.w.} akamwambia basi inatosha,na huku Sayyidna Muhammad {s.a.w.} mbora wa viumbe vyote anabubujikwa na machozi.
Huyo ndiye Ibin Masoud{r.a.},na huo ndio msimamo wake dhidi ya wazushi,na uzushi.

## KHATIMA

Mwisho wa makala hii tunahitimisha kwa kutaja vipengele muhimu vya sheria,ili vikusaidie ndugu yangu muislamu kupambana na bidaa na watetezi wake popote pale ulipo,ili uweze kuwatibu ndugu zetu ambao wameathiriwa na gonjwa hili hatari la uzushi katika dini,gonjwa ambalo limesababisha kudhoofika umma wa kiislamu kwasababu ya kuleta far'ka na mpasuko katika safu zao,na ndipo maadui wakaitumia fur'sa hii kuwatweza na kuwadhalilisha waislamu

*muongozo wetu katika dini ni Qur'an na Sunna za mtume{s.a.w.} kama walivyo fahamu maswahaba{r.a.} na waliowafuatia wao kwa wema.

*jua ndugu yangu muislamu kwamba jambo lolote la dini ambalo hakulifanya Bwana Mtume{s.a.w.} wala hakulifundisha, pamoja na

kwamba kulikuweko na sababu ya kulifanya jambo hilo,na wala hakukuweko na kizuizi chochote kilicho mzuia,
kulifanya jambo hilo baada ya kuondoka yeye{s.a.w.}ni kuzusha katika dini jambo lisilo kuwemo,na kufanya hivyo ni upotevu unaopelekea kuingia motoni,amesema Mtume{s.a.w.};

[..tahadharini na mambo ya uzushi-katika dini- kwani kila lenye kuzuliwa-katika dini- ni bidaa,na kila bidaa ni upotevu,na kila upotevu ni motoni].mfano wa jambo hilo ni kama kuweka adhana kwa ajili ya swala za eid,na kuzusha mikusanyiko ya maulidi.

*kuyawekea mifumo/utaratibu mambo ya dini tofauti na utaratibu wa kisheria ni kuzusha katika dini yasiyo kuwemo,amesema Mtume{s.a.w.};

[mwenye kuzusha katika dini yetu hii jambo lisilo kuwemo basi jambo hilo ni lenye kurudishwa]. Halitokubaliwa.kama kuweka utaratibu/mfumo maalumu wa kumdhikiri Allah {s.w.},au utaratibu/mfumo maalumu wa kumswalia mtume{s.a.w.} na kumsherehekea bwana huyu.

*Jambo lolote lile la dini ambalo maswahaba{r.a.} wamelifanya baada ya kuondoka bwana mtume{s.a.w.} kwa kupatikana sababu au kwa kuondoka vizuizi vilivyomzuia mtume{s.a.w.} katika uhai wake,kulifanya jambo hilo si bidaa,bali ni sunna,kama kuiandika Qur'an katika msahafu mmoja, kuindeleza swala ya tarawehe kwa jamaa,kuwapigavita walioritadi na kuzuia zaka.

*Bidaa zote katika dini ni mbaya na ni upotevu,na hakuna bidaa nzuri,na bidaa haiingii katika mambo ambayo si ibada kama vile kupanda ndege,gari,baiskeli,na n.k. amesema mtume{s.a.w.};[Nyinyi mnajua zaidi mambo ya dunia yenu].

hivyo  basi siyo sahihi kwa wazushi katika dini wanapokatazwa kuzusha katika dini haraka wao wakaanza kujitetea ooh! Kama kila kilichozushwa ni bidaa,na kila bidaa ni upotevu,basi magari ni bidaa pikipiki bidaa,feni bidaa,busati bidaa,ac bidaa,computer bidaa!

hii inaonyesha wazi kwamba ima hawaijui ni nini maana sahihi ya bidaa kisheria, au wanaijua lakini lengo lao ni kutaka kuwapoteza watu,au wanasifa zote mbili.

*Mwisho tunasema kwamba mikusanyiko ya maulidi ni haramu tena ni uzushi mbaya katika dini,na uzushi ni ugonjwa mbaya ulioleta far'ka katika umma wa kiislamu hivyo basi.haifai kwa waislamu kuyafanya mambo hayo baada ya kujua,ama wazee wetu na masheikh zetu waliotangulia mbele za haki,mwenyezi mungu -Inshaallah- atawasamehe sababu ni kwamba ukweli ulikuwa haujawadhihirikia,ama wewe uliye dhihirikiwa na haki kisha ukaipiga teke,ujuwe kwamba huna hoja ya kujieleza mbele ya Allah {s.w.t.},na ninakuhusia usijipe sifa za washirikina wa Makka,wao walikuwa wakijiliwa na jambo la haki hulipiga teke na huku wanasema hivi;

[Hakika sisi tumewakuta wazee wetu juu ya mila hii na sisi ni wenye kufuata athari zao.]

Huu ndio mwisho wa makala hii namba 1 bila shaka ndugu yangu umepata faida kwa kusoma makala hii kwahiyo tunaomba dua zako za kheri kwa muandishi na wote waliosaidia kuitawanya makala hii mpaka ikakufikia bila kusahau kuwaombea waislamu wote.

na ufahamu kwamba ukamilifu ni wa Allah {s.w.t.} peke yake na hakuna mwana adamu asiyekosea ila Manabii waliolindwa na Allah s.w.t.

**1)Athari mbaya ya uzushi katika uislamu.**

**(ndiyo hii iliyo mikononi mwako).**

**2,3)Athari mbaya ya uzushi katika uislamu.**

**4,5,6)Uharamu wa kuyajengea makaburi.**

,وصلى الله وسلم وبارك على سيدنا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين

.والحمد لله رب العا لمين